**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
# BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO
## ULYANKULU VTC
## 2025

Simu: +255784506652 P.O.BOX 111 ULYANKULU

Nukushi: ulyankuluvtc@gmail.com
www.veta.go.tz

Kumb. Na; 3/12/2024

Ndugu

.................................................................................

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA ULYANKULU Mwaka 2025**

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika
   Fani ya ..................................................
   Katika ngazi Level One
   mwaka wa 1 Boarding / Day
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 13/01/2025
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi. Kama fedha za tahadhali (caution Money) hazikutumika zitarudishwa
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

______________________________

JAPHARY BURTON MWAMBETE

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

# KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI VETA ULYANKULU- 2025 (LEVEL 1)

## 1. MAHALI CHUO KILIPO NA JINSI YA KUFIKA CHUONI

**Mahali chuo kilipo**

Chuo cha ufundi stadi VETA ULYANKULU, kipo Mkoani Tabora, Wilaya ya Kaliua, Tarafa ya Mwongozo, Kata ya Milambo, Kijiji cha Kaswa (barabara ya 13). Chuo kipo umbali wa KM97 kutoka Tabora, KM 60 Kutoka Urambo, KM 103 kutoka Kahama na KM 100 Kutoka Kaliua

Kutoka Tabora unapanda gari ziendazo Ulyankulu unashuka Ulyankulu (mwisho wa gari), Kama utakuwa unatokea Kahama pia unapanda gari ziendazo Kaliua/Mwamnange unashuka Ulyankulu (barabara ya 13), Ukitokea Urambo unapanda gari ziendazo Ulyankulu

a) **Hali ya hewa na mazingira ya chuo.**
Mazingira na hali ya hewa Chuoni Ulyankulu ni ya joto la wastani mchana, na baridi kidogo nyakati za jioni. Kwa hali hii wanachuo hawalazimiki kubeba nguo za kujikinga na baridi kali wajapo chuoni.

## 2. MAELEKEZO KWA AJILI YA USAJILI

I. Chuo kitafunguliwa tarehe **13/01/2025.** Mafunzo yatachukua muda miaka miwili (2). Mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe **24/01/2025**.
II. Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uje na kitambulisho au Namba ya NIDA, nakala ya cheti cha kuzaliwa na nakala za vyeti vyako vya kitaaluma, pamoja na barua hii.
III. Unatakiwa uje na fomu utakayojaziwa cha Daktari wa hospitali inayotambuliwa na Serikali kuthibitisha kuwa una afya njema ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa. (Fomu ya vipimo imeambatanishwa).
IV. Unatakiwa ufike na picha tatu za pasipoti (Passport size)
V. Unatakiwa kuthibitisha wewe pamoja na mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo katika fani uliyo pangiwa.

***Zingatia***

- Kwa mwanafunzi wa Bweni kama ana Bima hatolipia tena gharama za bima
- Mwanafunzi ambae hatokamilisha Ada, Michango na mahitaji yote yaliyoagizwa hatopokelewa Chuoni.
- Kumbuka kuandika jina kamili la mwanafunzi na kozi husika kwenye karatasi (risiti) ya malipo na kuipeleka kwa Msajili wa Wanafunzi mara moja umalizapo malipo.

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

## GHARAMA ZA MAFUNZO NA MICHANGO MINGINE

| S/N | Aina ya malipo | MUHULA WA I-2025 | | MUHULA WA II- 2025 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | BWENI | KUTWA | BWENI | KUTWA |
| 1 | Ada ya Mafunzo | 120,000 | 60,000 | 00 | 00 |
| 2 | Fedha za Uniform (suruali 2) | 40,000 | 40,000 | 00 | 00 |
| 3 | Overcoat/overoll moja | 30,000 | 30,000 | 00 | 00 |
| 4 | Ada ya Mtihani (CBA) | 00 | 00 | 25,000 | 25,000 |
| 5 | Tshirt | 15,000 | 15,000 | 00 | 00 |
| 6 | Fedha ya Ukarabati (Hairudishwi) | 20,000 | 20,000 | 00 | 00 |
| 7 | Godoro pamoja na Neti | 20,000 | 00 | 00 | 00 |
| 8 | Michezo | 10,000 | 10,000 | 00 | 00 |
| 9 | Nembo ya VETA | 5,000 | 5,000 | 00 | 00 |
| 10 | Kitambulisho | 5,000 | 5,000 | 00 | 00 |
| 11 | Kuchangia sherehe ya mahafali | 00 | 00 | 25,000 | 25,000 |
| | **JUMLA** | **265,000** | **185,000** | **50,000** | **50,000** |
| | MAHITAJI MENGINE UNAYOTAKIWA KUJA NAYO | | | | |
| 12 | Mashati mwawili (2) meupe ya tetron ya mikono mifupi | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 13 | Viatu vya Ngozi jozi moja (1) nyeusi | Uje navyo | Uje navyo | | |
| 14 | Nguo na Viatu vya Michezo (bluu) | Uje nazo | Uje nazo | | |
| 15 | Mathematical set, 1 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 16 | Scientific calculator, 1 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 17 | Vyombo vya kuogea, kufulia na kulia chakula | Uje navyo | - | | |
| 18 | Madaftari 07 makubwa, Quire 3 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 19 | Ream ya karatasi (A4) 1 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 20 | Spring file 1 | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 21 | Sweta la rangi ya Dark bluu | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 22 | Shuka 2 za bluu. | Uje nazo | - | | |
| 23 | Safety boot, Jozi moja (nyeusi) | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 24 | Jembe lenye mpini 1 | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 25 | Panga au Fyekeo 1 | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 26 | **Kitambulisho au namba ya NIDA** | Uje nayo | Uje nayo | | |

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

## TARATIBU ZA ULIPAJI ADA NA MAHITAJI MINGINE

Fedha yote ya malipo ya Ada na mahitaji mengine kwa Muhula wa kwanza italipwa kwa **mkupuo mmoja** kwa kutumia "**Control number**" utakazopewa na ofisi ya uhasibu ya VETA Ulyankulu. Mwaka wa kwanza bweni atalipa **Tsh 315,400/=** na Kutwa atalipa **Tsh. 185,000**. Muhula wa pili utalipa (**50,000**) elfu hamsini tu**/=**, "*Ni vema zaidi ukilipia benki au kwa wakala ambapo utapata RISITI ya karatasi*" inayohifadhika kirahisi.

Bima ya afya ni hitaji la lazima kwa wanachuo wote, Kwa wasio na kadi za Bima ya afya (NHIF) waje na fedha ***Tsh.50,400/=*** maalumu ya kulipia malipo ya bima ya afya kupitia Control number itakayotolewa na NHIF. Pia hakikisha unakuja na **Kadi au Namba ya NIDA** ili uweze kukatiwa BIMA ya Afya. Usipokuja nayo hutapokelewa.

Kwa wale wenye kadi za bima hakikisha kadi yako haijaisha/kukaribia kuisha muda wake wa matumizi na utahitajika kuionyesha kwa msajili wa Chuo ili ihakikiwe (Kadi ya Bima inayokubalika ni NHIF pekee ) hii ni kwa mujibu wa sheria za serikali kwa vyuo vyote, kadi hii itakuwezesha kupata huduma popote Tanzania,

## ZINGATIA:

1. Ukifanya makosa wakati wa malipo, pesa iliyolipwa hairudishwi.
2. Hutapokelewa/kusajiliwa kama huna kadi ya NIDA au bima ya afya (NHIF) inayofanya kazi au fedha taslimu tsh 50,400 kwa ajili ya malipo ya bima ya afya. Ili kuepuka usumbufu wa kurudishwa nyumbani, kwa wenye kadi za NHIF hakikisha unaihakiki kadi yako kwenye ofisi za Bima au kwenye vituo vya afya vinavyotumia kadi za NHIF kabla hujaja kuripoti chuoni.
3. Malipo ya bima ya afya ya (Tsh 50,400/=) yanalipwa kila mwaka.
4. Hutapokelewa kama hujalipa ada na mahitaji mengine yaliyoainishwa hapo juu.

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

**SHERIA ZA CHUO KWA MWANAFUNZI WA BWENI NA KUTWA:**

ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO: -

1. **MAHUDHURIO:**
   (a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1:15 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. ADHABU KALI ITATOLEWA KWA WACHELEWAJI.
   (b) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda Nyumbani, Hospitali Au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na Mwalimu wa zamu kupitia kwa Mwalimu wa darasa.
   (c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.
   (d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo.
   (e) Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.
2. **MAVAZI:**
   (a) Sare ya chuo ni suruali ya bluu na shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.
   (b) Ovaroli na overcoat zivaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.
   (c) Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.
   (d) Wakati wa kazi za vitendo mwanafunzi anatakiwa avae viatu vya Usalama (safety booty)
   (e) Viatu vya kuvaliwa madarasani ni viatu vyeusi vya ngozi, vyenye visigino vifupi na vinavyofungwa na Kamba
   (f) Soksi rangi Nyeusi kwa wavulana na Nyeupe kwa wasichana
3. **USAFI WA MWILI:**
   (a) Hairuhusiwi kuvaa Heleni, Pete, Bangili, Mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.
   Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.
   (b) NYWELE KWA WAVULANA:
      i. Zikatwe ziwe fupi sana, **KIPARA** hairuhusiwi kabisa.
      ii. Ndevu aina zote (mustachi/sharubu) haziruhusiwi.

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

(c) NYWELE KWA WASICHANA:

i. Zikatwe ziwe fupi sana au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma isiyozidi saba (7).
ii. ii. Kucha zisifugwe kabisa wala kupakwa rangi

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:**

(a) Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya Chuo au mwanafunzi mwenzake, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

(b) Ukipoteza kifaa cha Chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. **UGOMVI:**

Ugomvi kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja ikiwemo kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

6. **ULEVI:**

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kuchukua hatua za kisheria moja.

7. **MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na Mwanafunzi au kati ya Mfanyakazi na Mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atachukuliwa hatua kali za kisheria.

9. **LUGHA**

Lugha inayotumika kuendesha masomo ni Kiswahili.

10. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja

11. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wołe wa vipindi.

12. Mwanafunzi ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:

i. Jumamosi kuanzia saa 7:300 mchana hadi saa 12: jioni

ii. Jumpili kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12: jioni

- Ruhusa ya kutoka, Mwanachuo ataandika jina kwenye kitabu cha kutoka na kuingia sambamba na muda husika.
- Hairusiwi kutoka nje ya Chuo wakati wowote bila kibali maaluum.

13. Mwanafunzi yeyote anaeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha chuo na atajiandikisha lango Kuu na sare ya chuo. Mwanafunzi atayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuwa na kitambulisho au kibali atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa Chuo kabisa.
14. Mwanafunzi atakayepatikana na kosa la kulala nje nje ya chuo bila kibali atasimamishwa Masomo.
15. Haitaruhusiwa kupika chakula bwenini, na atakayekiuka sharia atachukuliwa hatua kali.
16. a) Ni marufuku Mwanchuo wa kike na wa kiume kutembeleana mabwenini

    b) Hairuhusiwi kabisa kwa mwanachuo kuingia eneo wanamoishi wafanyakazi bila ruhusa au kibali maalumu.
17. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa Zamu itatolewa.
18. Taa za madarasani na Mabwenini zizimwe saa 4:00 usiku
19. Hakuna ruhusa kumkalibisha au kumlaza mgeni yeyote Bwenini, ikiwa Mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku za masomo ni lazima kumjulisha Mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha

    Mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha sehemu ya mazungumzo.
    - Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila jumamosi kuanzia saa 7 mchana hadi saa 12:00 jioni.
    - Kila jumapili na sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.
20. Vyumba vya Madarasa na Vifaa vitumiwe kulingana na matumizi au shughuli zake na si vinginevyo. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za Majengo ya Chuo.
21. Hairuhusiwi kulala nje ya Chuo. Iwapo italazimika ruhusa itatolewa na Ofisi ya Mkuu wa Chuo.

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

---

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY
## ULYANKULU VOCATIONAL TRAINING CENTER (ULYANKULU VTC)

### REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Admission to ULYANKULU VTC is conditional upon receipt of satisfactory medical report. The practitioner to whom this form is presented is requested to examine the candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an………………….................. (Trade)

The Medical Officer
……………………………….
……………………………….
……………………………….
……………………………….
Please examine …………………………………………….... (candidates name)

(i) Eyesight………………………………………………
(ii) Hearing……………………………………………….
(iii) Height…………………………………………..…..
(iv) Allergies………………………………………………
(v) Weight……………………………………………….
(vi) Asthma……………………………………………….
(vii) Epilepsy………………………………………………
(viii) Other serious diseases……………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that/she is physically fit/unfit for training as above.
TITLE………………………………………SIGNATURE………………………..
Official Stamp………………………………… Date…………………………….

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

**TAARIFA YA MWANACHUO (PERSONAL PARTICULARS)**

| AFFIX YOUR PASSPORT SIZE HERE<br>BANDIKA PICHA YAKO HAPA<br>(Mwanafunzi) |
|---|

**SEHEMU (A)**

Ijazwe na mwanafunzi (tumia herufi kubwa)
1. Jina la ukoo Bw./Bibi/Bi……………………………………………
2. Majina mengine……………………………………………………………
3. Mahali ulipozaliwa (Wilaya)……………………………..Mji/Kijiji…........
4. Kiwango cha elimu………………………
4. Tarehe na mwaka wa kuzaliwa…………………………………………………
5. Hali ya ndoa………………………(umeoa/olewa)
6. Anuani ya makazi ya kudumu………………………………………………..
7. Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………
8. Anuani ya mzazi/mlezi…………………………………………………………...
……………………………………………………………………………………
9. Nambari ya simu ya mzazi/mlezi……………………………………………………………

**Uthibitisho**
Mimi …………………………………………………… Nathibitisha kwamba, ninaikubali nafasi hii, na kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni sahihi na za kweli.
Sahihi………………………………… Tarehe…………………………………

**SEHEMU (B)**

Ijazwe na Mzazi/Mlezi/Mdhamini
Mimi …………………………………… S.L.P. ……………………………………………
Simu ya mkononi……………………………………………
Ninathibitisha kuwa ninamdhamini mtajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za Mafunzo (ada) n.k. pamoja na nauli wakati wote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo.
Tarehe……………………………... Sahihi……………………………………
Uhusiano……………………………………………………………...